**Title: Under the Mango Trees**

**EPISODE 7**

**Author: Romie Singh**

**Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun**

**List of characters for episode 7:**

- Narrator
- Desirée
- Lorraine
- Sazi
- Eric
- Alice
- Bongo
- Children in background

**INTRO**

Hujambo na karibu kwenye sehemu ya saba ya kisa kwa jina Chini Ya Miembe katika mfululizo wa mchezo wa kuigiza katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako, mchezo unaoangazia mengi kuhusu mpango wa uzazi, hususan kwa vijana. Leo hii Eric anatafakari juu ya kazi yake baada ya masomo na pengine maisha yake ya baadae huku dada yake pacha Lorraine na mpenzi wake Sazi wanajadiliana kuhusu mpango wa uzazi.

SIG.TUNE UP HOLD UNDER AND FADE

**NARRATOR:** Kaka yake Lorraine, Eric, alipogundua kuwa wazazi wake wana nyumba katika kijiji cha Mtelera, na pia kuwa mama yake atasimamia kliniki ya kijiji hicho.basi alianza kupanga mpango akilini mwake.

**<u>Sc. 1 Interior.</u>**

**SFX: Kitchen sounds**

**1. ERIC:** Je unaonaje kama ningepata ujuzi kwa kipindi cha mwaka mmoja katika kliniki ya Mtelera kabla sijaanza Chuo?

**2. ALICE:** Ni sawa. Hilo ni wazo zuri, Eric!

**3. ERIC:** Hata siamini kama tuna nyumba kule! Lo. Ni vizuri sana!

**4. ALICE:** Tunaweza kuhamia mara tu itakapomalizika kupakwa rangi**.** Utakuwa karibu na Desirée na familia yake. Nadhani atafurahi sana! Hata wewe pia , eh, Eric?

**5. ERIC: (laughing softly)** Ni kweli mimi pia, Ma! Na nitafanya kazi kwa bidii.

**6. ALICE:** Nina hakika kwa hilo. Je baadae? Una mpango wa kujiunga na chuo cha tiba cha St. Michael cha Granville?

**7. ERIC:** Ndio, na baada ya kupata ujuzi nitakuwa tayari nimetimiza nusu ya sifa zinazotakikana kuingia chuoni!

**8. ALICE:** Unajua, idara ya Afya inahitaji mtafiti ambae atakusanya data za gharama za mpango wa uzazi. Tuseme, kutafuta ni mipango ipi ya uzazi ambayo serikali inaweza kugharimia kwa urahisi ili kuwafaidi wananchi. Ninaweza kukupa maelezo zaidi ukitaka.

**9. ERIC:** Mpango wa uzazi? Kwa hiyo ina maana Tembe na Kondomu, au siyo?

**10. ALICE:** Pia njia za sindano na hata Koili. Kuna njia zingine mpya za kupandikiza na pia tembe za mapovu. Serikali inahitaji kujua gharama ya kila njia na pili kujua kila jamii yaani mke na mume watatumia kiasi gani kwa muda wa mwaka mmoja. Mpango huu unaitwa MKJ maana yake Mwaka wa Kinga kwa Jamii. Kwa kimombo tunauita CYP yaani Couple Year of Protection.Mpango huo utakufaidi sana kielimu kwa kuwa utapata fursa ya kufanya kazi na wateja au wagonjwa, utakuwa unawahoji wewe mwenyewe yaani utakuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na wagonjwa.

| | | |
|---|---|---|
| **11.** | **ERIC:** | Lakini swali ni kwamba je watu wa kijiji cha Mtelera wanatumia kinga ya uzazi? Mbona, huko ni kijijini sana. |
| **12.** | **ALICE:** | Wanaume na wanawake wa huko walikuwa wakitumia njia za kienyezi kwa karne nyingi. Kwa mfano kujizuia kabisa kufanya mapenzi, njia hii inamtegemea mwanamume ili asimpe ujauzito mwanamke. Njia nyingine ni kunyoshesha kwa muda mrefu. |
| **13.** | **ERIC:** | Inanibidi niandike! Umesema kuhusu mtoto kunyonya maziwa ya mama kwa muda mrefu, sio? |
| **14.** | **ALICE:** | Kwa sababu homoni zinazo jengeka wakati wa kunyonyesha , zinamzuia mwanamke kupata hedhi kwa muda mrefu kadri atakavyo endelea kunyonyesha kwa hiyo hawezi kupata uja uzito. |
| **15.** | **ERIC:** | Ah!  ndio maana nawaona wanawake wengi wananyonyesha watoto wao mpaka hata wakiwa na miaka mitatu? |
| **16.** | **ALICE:** | Naam, na mambo hayo ndio utapaswa kuyafanyia utafiti ili uyafahamu mwanangu! Unajua ungefanya nini? Nenda ukamuhoji nyanya Linda! Bella pia, kwa sababu anaishi |

na mpenzi wake muulize kwa nini hajapata mtoto mpaka sasa. Na pia usimsahau dada yako mwenyewe!

**17. ERIC:** Lorraine? Sawa. Hilo ni wazo zuri. lakini Ma, mimi ni mwanaume. Tena kijana bado. Unadhani wanawake watataka kuzungumza na mimi kuhusu maswala ya mpango wa uzazi?

**18. ALICE:** Hapo umesema kweli. Wanawake hawatafurahia kuzungumza nawe hadi pale utakapo kuwa umehitimu udaktari kama vile baba yako. Lakini kuvaa lile koti jeupe la daktari kutakusaidia sana, usijali unaweza kuazima la kwangu!

**19. ERIC: (laughing)** Basi nitajaribu. Unajua naweza kuwa naandika maelezo wakati wa mahojiano na nikamtumia Desirée kufanya mahojiano hayo. Kwa sababu kwanza yeye ni mwanamke tena anatoka katika jamii hiyo ya Mtelera, anaizungumza vyema lugha ya huko. Wow! Tutakuwa na timu nzuri kweli. Ngoja nitamuuliza!

**NARRATOR:** Kliniki inatarajiwa kufunguliwa katika kipindi cha wiki tatu. Upande mwingine, dada yake Eric, Lorraine, akumbwa na wasiwasi kwa kuwa mashindano ya Pop Idols yanaanza pia katika muda wa wiki tatu

lakini hajisikii vyema. Pia Sazi pia amegundua mabadiliko katika hali ya mpenzi wake.

**<u>Scene 2 Interior.</u>**

20. **SAZI:** Jana ulikuwa umechoka, leo pia hali ni hiyo hiyo bado umechoka, Lorraine, mpenzi una nini?

21. **LORRAINE: (irritated)** Hata najisikia vizuri , Sazi. Tafadhali usikuze mambo! Ni wasiwasi tu. Mashindano ya Pop idols karibu yataanza na nyimbo ni nyingi tena zote nzuri hata sijui nitachagua ipi. Yaani nimeshindwa kuamua.

22. **SAZI:** Na Bongo anapendekeza nini? Yeye ni ajenti wako lakini.

23. **LORRAINE: (irritated)** Ndio nitaonana nae baadae. Sasa wacha kuzungumza hebu niache nifanye tena mazoezi ya nyimbo yangu ya kwanza.

24. **SFX: Starts singing.**
25. **SFX Paper/plastic rustle**

26. **SAZI:** Lorraine? Ni nini hiki?

27. **LORRAINE:** Nini? Kuna nini, Sazi?

**28. SAZI:** Mpenzi? Hii paketi inaonyesha kuwa tembe yako ya leo ni ya siku ya alhamisi lakini leo ni ijumaa. Ina maana kuwa ulimeza tembe mara ya mwisho siku ya jumatano asubuhi. Umechelewa siku moja mpenzi.

**29. LORRAINE: (subdued)** Oh, ni kweli, um, lakini hiyo ni pakiti ya mwezi uliopita. Nilisahau kumeza tembe siku moja kwa bahati mbaya, lakini nilianza pakiti mpya mara nilipogundua.

**30. SAZI:** Ukweli ni kwamba ulikosa kumeza tembe yako siku moja mwezi uliopita.

**31. LORRAINE:** na mimi nasemaje, basi wacha chokochoko! **(Softer)** Njoo mpenzi wangu Sazi, nataka unisaidie kuchagua ni wimbo upi nitakaoimba kwenye mashindano ya mchujo.

**NARRATOR:** katika kijiji cha Mtelera, Desirée aliongeza bidii ya kutaka kujua mjomba wake Blessing yuko wapi?. Aliahidi kuwa atakuja kuwachukua watoto wake. Lo! Angefanya hivyo kwa kweli angempunguzia mzigo mkubwa. Lakini je. Baba yake nae yuko wapi? Alitaka sana kumpata pia kwa ajili ya mdogo wake Endurance ambae anamuulizia baba yao kila siku. Eric aliahidi kumsaidia.

**32. SFX: Cell ring tone**

**33. ERIC: (FX:Phone)** Hallo Des. Ni mimi, Eric. Hujambo?

| | | |
|---|---|---|
| **34.** | **DESIRE:** | Eric! Hallo. Mimi sijambo na wewe je? |
| **35.** | **ERIC:** | namimi naendelea vizuri. Vipi mambo? Kuna habari yoyote? |
| **36.** | **DESIRE:** | Aah, nyanya hajui anuani kamili ya baba lakini anasema ana gereji katika barabara moja kubwa huko Mashariki. |
| **37.** | **ERIC:** | Vizuri sana! Hiyo inamaanisha basi atakuwa na simu lazima. |
| **38.** | **DESIRE:** | Ndio, na mjomba Blessing huwa anawasiliana nae mara nyingine. Kwa hivyo tukimpata baba yangu bila shaka tutampata mjomba Blessing pia. |
| **39.** | **ERIC: (FX:Phone)** | Nadhani itakuwa rahisi sasa! Baba yangu amesema tunaweza kukaa nae mjini Granville wakati wowote tutakapo taka. Sasa ni wewe tu useme lini uko tayari! Shule zinafungwa wiki ijayo unaonaje tunaweza kwenda wakati huo? |
| **40.** | **DESIRE:** | Ni sawa. Lakini ukumbuke kuwa wiki hiyo itakuwa na shughuli nyingi. Kwa sababu mashindano ya Pop Idols ndio yatakuwa yanaanza na Lorraine anashiriki. Ikiwezekana |

tunaweza kwenda kumtafuta babayangu na mjomba Blessing mchana halafu twende kwenye mashindano jioni. Ni lazima tumuunge mkono Lorraine.

**41. ERIC:** Oh, wow. Kweli Lorraine anashiriki hata nilikuwa nimesahau! Ok.Unafanya nini sasa?

**42. DESIRE:** Namtarajia dada yangu Bella wakati wowote kutokea sasa. Anakuja kunifundisha kuoka Keki! Ikiwa una nafasi unaweza kuja kuionja hiyo keki, karibu sana! Japo kuwa nafahamu kuwa ni safari ndefu, tena hasa sababu yenyewe ikiwa ni kuonja keki tu.

**43. ERIC:** Keki sio sababu peke yake mimi nataka kuja, Des. Nina mengi nitakayo kukueleza. Des, ni mambo mazuri na ningetaka kuzungumza na Bella pia. Basi nitegemee kwenye milango ya saa kumi hivi. Sawa?

**44. DESIRE:** Sawa! Mambo gani hayo unayotaka kunieleza. Eric? Uh? (Laughing)

**45. MUSIC UP**

**NARRATOR:** Wakati Eric alipokuwa anajiandaa kwenda kumtembelea Desirée, mchana huo huo, Lorraine nae alikuwa anakwenda ofisini kwa

Bongo " Rainbow Agency" kwa ajili ya kuupitia mkataba ambao kiini chake ni kuwa, haki zake zote zitamilikiwa na ofisi hiyo kwa muda wa mwaka mzima iwapo atashinda kwenye mashindano hayo ya Pop Idols.

**46. BONGO:** Hallo, mpenzi! Hmmm. (Kiss on cheek) Hujambo? Mbona unaonekana dhaifu kidogo? Vipi una wasiwasi?

**47. LORRAINE:** Samahani, Bongo! Naomba kwenda msalani kidogo, chooni.

**48. BONGO:** Bila shaka, ni mlango mwekundu, mkono wako wa kulia.

**49. SFX: Off mic coughing/retching**

**50. BONGO: (businesslike)** Hey, Lorraine. Mimi nina kazi nyingi sana na naona kuwa huwezi kutia saini huu mkataba sasa hivi. Chukua nenda nao nyumbani ukausome vizuri. Lakini kumbuka siwezi kukusajili kwenye Pop Idols mpaka utakapo tia saini..

**51. LORRAINE:** La. La niko sawa , Nafikiri labda nilikula kitu ambacho kinaniletea tabu kidogo. Ninataka tuzipitie nyimbo zangu pamoja Bongo. Uliahidi kuwa utanisaidia kuchagua wimbo nitakao anza kuimba.

**52. BONGO:** Ok sawa. Hebu nisikie.

**53. SFX: Lorraine starts an up-tempo pop song. Suddenly stops and breathes very fast**

**54. BONGO:** Lorraine? Nini mbaya, una shida gani? Mbona unakosa pumzi za kuimba wakati kama huu?

**55. LORRAINE:** Nasikia roho inanichafuka, Bongo. Lazima kitakuwa chakula nilichokula mchana.

**NARRATOR:** Lakini hali yake ilizidi kuwa mbaya. Hakutaka kufikiri nini hasa kinaweza kuwa.  Hata ingawa ndani ya moyo wake, Lorraine alijua kuwa kuna kitu kinaendelea mwilini mwake.

**OUTRO.**

Na mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa sehemu ya saba katika mchezo kwa jina Chini ya Miembe . Mfululizo wa michezo inayokujia katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako! Mchezo huu umetungwa na kuandikwa na Romie Singh. Mchezo huu unaangazia jinsi njia za mpango wa uzazi zinavyoweza kuwasaidia vijana kujenga maisha yao. Mpango wa uzazi unawapa fursa wanawake na wapenzi wao kuamua wakati muafaka wa kupata mtoto. Usikose kujiunga nasi katika sehemu ya nane ambapo Eric anavumbua njia zaidi za kumfanya awe karibu na Desirée. Matumaini ya Lorraine ya kuwa nyota wa Pop Idol yanaanza kuyumba yumba. Kumbuka unaweza kuusikiliza tena mchezo huu. Tutumie pia maoni yako na mwambie rafiki yako ausikilize pia anuani ya mtandao wetu ni : d w world dot d e mkwaju l b e
Hadi wakati mwingine, kwaheri.

**56.** SIG TUNE

**END OF EPISODE SEVEN**